**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MTAMA**


**MKOA WA LINDI,**
**SIMU: 0717404471**
**: 0757246378**
**E-Mail: mahiwa1995@gmail.com**

**SHULE YA SEKONDARI MAHIWA**

**S.L.P 129**

**MTAMA- LINDI**


**TAREHE…………………………………**

**KUMB: NA.B.64/MAH/SS/FKT/2022/2023**

**MZAZI /MLEZI WA………………………………………………………**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MAHIWA**

1. Jumuiya ya shule ya sekondari Mahiwa inayofuraha ya kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika Shule ya Sekondari Mahiwa, mwaka wa masomo 2022/2023. Hongera sana. Shule ya sekondari mahiwa ipo umbali wa kilometa 82 kutoka makao makuu ya mkoa wa Lindi.

2. Kutoka Lindi mjini kuelekea Masasi ,Mwanafunzi anatakiwa kushuka **kituo cha mabasi Nyangao** na kukodi pikipiki kuelekea shule ilipo, umbali wa kilometa nne (4) kutoka Nyangao

3. Muhula wa masomo utaanza tarehe ............................Mwanafunzi anatakiwa kuripoti hapa shuleni tarehe…………………………………Mwisho wa kuripoti ni tarehe……………….. Fika na mahitaji yote yaliyoanishwa.

**Unakaribishwa sana tarajia kupata unachokijia kwa kuwa Mazingira ni rafiki sana kwa usomaji.**

4. **Mambo Muhimu ya kuzingatia:**

**2.1: Sare ya shule.**

**(a) WASICHANA**

- Sketi ndefu mbili rangi ya kijivu mpauko zenye V mbele isiyobana na isiwe na mpasuo
- Shati mbili nyeupe mikono mifupi aina ya Tomato(wanaovaa Hijabu, nusu kanzu mbili na shungi nyeupe ndefu yenye kusitiri mikono na kifua)
- Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na visigino virefu na viwe vya kufunga kwa kamba
- Soksi nyeupe ndefu jozi mbili au zaidi.

**Nguo za kushindia na shamba dress:**

- Sketi nyeusi mbili isiyobana na isiwe na mpasuo
- Tshirt mbili (2) za cream ambazo zina nembo ya shule (Zinapatikana shuleni) kwa wanaovaa hijabu (hijabu iwe rangi ya zambarau) kwa ajili ya kazi za shamba
- Track suit rangi ya kijivu kwa ajili ya michezo
- Raba za kukimbilia mchakamchaka ni **lazima** kuja nazo.

**(b) WAVULANA:**

- Suruali mbili ndefu rangi ya kijivu mpauko, mbele iwe na rinda na chini iwe na mkunjo" turn up" na upana wa wastani .(Isiwe na mitindo kama vile, Modo, jeans style)
- Shati mbili mikono mifupi (aina ya Tomato)
- Mkanda mweusi wa ngozi
- Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyo na visigino virefu na **visiwe** buti.
- Soksi nyeupe ndefu jozi mbili au zaidi

**Nguo za kushindia na shamba dress**

- Suruali nyeusi mbili
- Tshirt mbili cream zenye nembo ya shule(zinapatikana shuleni).
- Track suit rangi ya kijivu kwa ajili ya michezo
- Bukta ya bluu na fulana ya bluu na viatu vya michezo. Raba za kukimbilia mchakamchaka ni **lazima** kuja nazo.

**NB: Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani. Muda wote atavaa nguo za shule zilizoagizwa. Aje nazo za kutosha ,Hata zaidi ya idadi iliyotajwa.**

5. **MALIPO NA MAHITAJI MENGINE YA SHULE**

**A. (i) ADA**

| MAHITAJI | KIASI | MAELEZO |
|---|---|---|
| ADA | 70000/= | Mwaka Mzima |

**NB**:Inaweza kulipwa 35000/= kila muhula

**(ii) MALIPO MENGINE YA SHULE**

| MAHITAJI | KIASI CHA FEDHA | MAELEZO |
|---|---|---|
| Tahadhali | 5,000/= | Mara moja haitarejeshwa |
| Mpishi,Mlinzi na watumishi wengine | 30,000/= | Mwaka mzima |
| Kitambulisho, nembo | 8,000/= | Mara moja |
| Ukarabati, | 15,000 /= | Mara moja |
| Usafiri kwa wanafunzi wagonjwa | 10,000/= | Kila mwaka |
| Taaluma | 20,000/= | Kila mwaka |
| Mitihani ya kujipima (UTAMILIFU) | 20,000/= | Kidato cha tano |
| JUMLA | 108,000/= | |

**NB: MALIPO YOTE YA FEDHA YALIPWE KWENYE AKAUNTI YA SHULE KAMA IFUATAVYO:**

**NAMBA YA AKAUNTI**: **NMB 70201200056**

**JINA LA AKAUNTI: MAHIWA SECONDARY SCHOOL**

**B. MAHITAJI MENGINE;**

Mwanafunzi anapokuja shuleni aje na vifaa vifuatavyo:

- Ream moja plain A4 (kila Muhula)
- GRAPH PAD mbili (kila muhula)
- Sanduku imara la chuma na kufuli,(Tranka)
- Blanket moja (kwa wenye matatizo ya kiafya),Foronya 1,Chandarua 1( rangi ya bluu bahari)
- Mashuka mawili ya rangi ya PINKI
- Vitabu vya masomo ya Tahasusi angalau kimoja kwa kila somo.
- Scientific calculator kwa wanaosoma Geography, Chemistry,Physics na Mathematics.
- Dissecting kit kwa wanafunzi wa CBG na PCB
- Vyombo vya chakula (sahani ,bakuli, kijiko na kikombe) vya plastiki
- Ndoo mbili (moja kubwa kwa ajili ya jikoni na ndogo kwa ajili ya matumizi yake)
- Kwanja 1,jembe1, reki 1, panga 1 na fagio ya ndani 1(VIWE NA MIPINI)
- **KILA MWANAFUNZI AJE NA BIMA YA AFYA INAYOTUMIKA HOSPITALI YOYOTE TANZANIA.(KAMA HUNA BIMA YA AFYA, NJOO NA PESA TSH 50,400/= NA PICHA 3 ZA PASSPORT SIZE)**

- Passport size 4 za wazazi au ndugu wakaribu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba za simu.
- Tochi ya betri
- Dawa ya chooni dumu moja la lita 5.
- Godoro 2 ½ x 6
- Net ya blue bahari 2 ½ x 6
- Mwanafunzi wa HGK, CBG na PCB aje na hardbroom 1 yenye mpini mrefu.
- Mwanfunzi wa HGLna PCM aje na brush za chooni na moper (SQUEEZER)

**MATIBABU.**

Taarifa za matatizo ya Afya zitolewe mapema na mwanafunzi kwa Mwalimu wa Afya kwa ajili ya utaratibu wa matibabu. Endapo mwanafunzi atalazwa hospitalini atarudi mara tu atakaporuhusiwa na daktari na kuripoti kwa mwalimu wa Afya**.**

**VIFAA VYA USAFI BINAFSI**

Mwanafunzi aje na sabuni,taulo,kandambili,rangi ya viatu vyeusi, mswaki , dawa ya mswaki, Mafuta ya kupaka na nguo za ndani, Mafuta ya kupaka aina ya **Cream na marashi haviruhusiwi**

**MWENENDO NA TABIA**

- Kila mwanafunzi anawajibu wa kuonyesha kiwango cha juu cha nidhamu katika kila shughuli kama vile kuwahi,ukakamavu,usafi,uaminifu,michezo na kila jambo linalomuhusu.
- Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu na kuwatii walimu,wafanyakazi wasio waalimu wageni na walezi wengine shuleni na nje ya shule.
- Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu viranja wa shule walioteuliwa na kuchaguliwa na wanafunzi wenzake ndani na nje ya shule.

**NJE NA NDANI YA MIPAKA YA SHULE**

- Hairuhusiwi kwenda nyumba za walimu na watumishi wasio walimu bila ruhusa au sababu za msingi.
- Hairuhusiwi kuingia kwenye kumbi za starehe( baa, virabu vya pombe na nyumba za kulala wageni.
- Hairuhusiwi mwanafunzi kulala na kutoka nje ya shule bila kibali cha mkuu wa shule wakati wowote.

## 6. MAMBO YALIYOPIGWA MARUFUKU SHULENI

- Kuonesha tabia mbaya kama vile kupigana,kupiga kelele ovyo, kutukana na ulevi wa aina yoyote
- Kukashifu dini ya aina yeyota au kabila la mtu
- Kushabikia chama chochote cha siasa
- Kuhamasisha migomo au vurugu ya aina yeyote
- Kukaribisha wageni pasipo idhini ya shule
- Kumkaribisha mgeni au mwanafunzi yeyote asiyehusika bwenini
- Kuharibu mali ya shule,Umma au mwenzako kwa makusudi
- Kuweka dawa nywele, kusuka nywele,kufuga kucha , kufuga ndevu na kuweka rangi kucha au nywele.
- Kuvaa nguo zisizoainishwa kwa matumizi hapa shuleni
- Kumiliki na kutumia SIMU, LINE ya simu au kifaa chochote cha kieletroniki katika mazingira ya shule.

## BAADHI YA MAKOSA YANAYOMFUKUZISHA SHULE MWANAFUNZI MARA MOJA

i. Wizi
ii. Uesharati
iii. Kutumia kileo cha aina yeyote
iv. Makosa ya jinai
v. Kupiga au kupigana
vi. Kuharibu makusudi mali ya umma
vii. Kudharau bendele ya Taifa, picha ya Raisi au Mwenge wa uhuru
viii. Kuolewa au kuoa
ix. Kugoma,Kuchochea na kuongoza mgomo
x. Kumiliki na kutumia SIMU au line ya simu shuleni
xi. Lugha ya matusi
xii. Kugoma na kukataa adhabu
xiii. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k

**PRESIDENT'S OFFICE,**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**Mahiwa secondary school**
**P.O.BOX 129**
**Mtama - Lindi**

REF: NO ……………………………..
To The Medical Officers (District/regional)
………………………………………………………..
Sir/Madam,

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION TO**
(***Name of student)……………………………………………………***

Please examine the above named student and give the report regarding his/her suitability for undertaking secondary school studies.

1. Student's full name……………………………………………………………………………
2. Blood…………………………………………………………………………………………..
3. Stool…………………………………………………………………………………………
4. T.B test ……………………………………………………………………………………..
5. Syphilis test……………………………………………………………………………………..
6. Urine examination……………………………………………………………………………..
7. Eyes test ……………………………………………………………………………………..
8. Chest test……………………………………………………………………………………..
9. Ears test…………………………………………………………………………………………
10. Spleen…………………………………………………………………………………………
11. Abdomen………………………………………………………………………………………
12. Pregnancy (for girls only)……………………………………………………………………

**ANY ADDITIONAL INFORMATION: EG Physical defects or impairment, infection, family diseases** etc

…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
COMMENTS:……………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………..

I certify that the above student is suitable/unsuitable for secondary school studies. If unsuitable give reasons

…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………

**Name of Medical Officer**…………………………………………………**Signature** ………………………
**Date**………………………………………………………………….. **Official stamp** ………………………………

# A. YAH: KUKUBALI/KUKATAA NAFASI (MWAFUNZI)

Mimi ………………………………………………………………………….. nakiri kopokea barua ya kujiunga na masomo ya kidato cha Tano katika shule ya sekondari mahiwa. Baada ya kusoma na kuelewa yaliyoandikwa katika fomu hii NIMEKUBALI NAFASI/NIMEKATAA NAFASI ya kuendelea na masomo.

Ninaahidi mbele ya mzazi/mlezi wangu kuwa nitazingatia kanuni, sheria na taratibu zote za shule. Kamwe sitoshiriki au kujihusisha na vitendo vya uvunjaji wa sheria za shule na makosa mengine ya jinai.

Nitatumia juhudi na maarifa katika kujifunza kwa manufaa yangu, wazazi, jamii na taifa kwa ujumla. Aidha niaahidi kuwepo shuleni muda wote na endapo itatokea nataka kutoka nje ya shule nitaomba ruhusa na kuvaa sare rasmi za shule.

Jina la mwnafunzi ……………………………………………saini …………………...tarehe……………………

Jina la mzazi/mlezi ……………………………………………saini…………………...tarehe……………………

A. MAKUBALIANO YA MZAZI/MLEZI.

Mimi ………………………………………….. Mzazi/mlezi wa mwanafunzi …………………..……… Wa kidato cha …………….. mwaka …………………... ninakubaliana na masharti tajwa hapo juu, hivyo naahidi kutekeleza mkataba huu na kuamuru mwanangu autekeleze. Endapo mwanangu atashindwa kutekeleza basi sheria ifuate mkondo wake.

**MAWASILIANO**

Mawasiliano yote yafanyike kwa namba za simu zifuatazo:

**MKUU WASHULE: 0757246378/ 0717404471**
**MAKAMU MKUU WA SHULE: 0713784869/0687967745**
**MWALIMU WA BWENI: 0712727965/0683650759**

Mwanafunzi anapaswa kujaza fomu ya matibabu na taarifa binafsi.

Ninakutakia safari njema ya kufika hapa shuleni. Karibu sana MAHIWA.

……………………………………

**HONORATI E TARIMO**
**MKUU WA SHULE**
**MAHIWA SEKONDARI**